

COUNTY GOVERNMENT OF LAMU



THE COUNTY ASSEMBLY OF LAMU
THE HANSARD

Wednesday, 3rd December, 2025

*The Assembly met at the
Main Chambers, at 2:30 p.m.*

[The Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna) in the Chair]

PRAYERS

[The Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]: Next Order.

Clerk-at-the-Table: Papers.

PAPERS

MCA Barisa Deko Bana (Basuba): Thank you Mr Deputy Speaker.

Mr Deputy Speaker Sir, I would like to table the following Papers on the floor of this House: -

1. Supplementary Annual Budget Estimates for the year ending 30th June 2026

Thank you.

[The Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]: Next Order.

Clerk-at-the-Table: Motion.

MOTION**PAYMENT OF SHA PREMIUMS FOR THE AWER AND SANYE MINORITY
COMMUNITIES**

MCA Barisa Deko Bana (Basuba): Thank you Mr Deputy Speaker.

Mr. Deputy Speaker Sir, I beg to move the following motion: -

AWARE THAT Article 43(1)(a) of the Constitution of Kenya guarantees every person the right to the highest attainable standard of health care services, including reproductive health care:

FURTHER AWARE THAT the Awer and Sanye communities are officially recognized as marginalised and minority groups residing in Lamu County, many of whom live in remote areas with limited access to economic opportunities and healthcare;

DEEPLY CONCERNED THAT a significant number of members from these communities are unable to afford premiums under the new Social Health Authority (SHA), formerly NHIF, thus facing serious difficulties in accessing medical care or paying hospital bills;

RECOGNISING THAT the County Government has a duty under the Fourth Schedule of the Constitution to promote health and protect vulnerable populations:

NOW THEREFORE, this Assembly urges the County Executive Committee Member for Health, in consultation with the Department of Finance and Social Services, to:

1. Identify and register all Awer and Sanye households in Lamu County in need of health coverage:

2. Allocate funds in the current or supplementary budget to fully cover their SHA premiums:
3. Establish a framework for sustainable and inclusive health insurance support for all other Indigent and marginalised groups in the county:
4. Table a report within 60 days detailing implementation progress and timelines.

Thank you.

Secunder

MCA Fahd Dini Adnan (Minority Leader): Asante Bwana Naibu Spika, nasimama kuunga mkono mswada huu. Kusema kweli jamii ya Awer ni ndogo na Maisha yao ni ya hali ya chini kwa hio ni vyema iwapo serikali itaipa jamii hii mtazamo wa kihuruma ili wao pia iweze kujismamia kiupande wa matibabu. Licha ya kuwa na SHA, itakuwa bora Zaidi wakiwa na zahanati yao ambayo itawapa huduma ya kwanza. Naomba Waheshimiwa wenzangu waunge mkono mswada huu ili jamii ndogo ndogo katika kaunti yetu ziweze kusaidika.

(Motion Proposed)

Member's Contributions

MCA John Mburu Gitonga (Hongwe): Asante Bwana Spika, nasimama kuunga mkono mswada huu. Jamii hii inajitegemea kimaisha na biashara zao huwa ni za kubahatisha na ikiwa watu hawa hawajasajiliwa kwa SHA, basi hakuna huduma ya matibabu wataweza kupokea katika hospitali za serikali. Bwana Naibu Spika, kwa saa hii ukitaka kujisajili na SHA, ni lazima uwe umelipa kiasi cha mwaka mzima ambapo si chini ya elfu kumi. Hii ni ngumu sana hususan kwa jamii kama hizo. Ikiwa serikali ya kaunti itaweza kutenga bajeti na kuwaingiza watu hawa katika SHA, basi pia takuwa imetusaidia na kuturahishishia sisi pia kama wajumbe.

MCA Aisha Ali Abdulrahman (Nominated): Asante Bwana Spika, nasimama kuunga mkono mswada huu. Kusema kweli, jamii ya sanye na boni wako katika hali mbaya sana. Jamii hii inaishi katika mpaka wa Kenya ambao kuna mambo mengi kuhusiana na usalama. Watu hawa kupata huduma za hospitali ni shida. Sisi kama wawakilishi wadi, tumeitengea jamii hio basari ili iwasaidie katika elimu. Kwa hivyo pia tunaomba serikali izingatie upande wa kupokea huduma za matibabu hususan kuwasajili na SHA. Sisi kama viongozi tusipowatetea watu hawa basi takuwa hatufanyi sawa. Kuna mfano mmoja ambao mama flani wa jamii hio alijisajili SHA lakini ikawa haifanyi kazi wakati huo na alikuwa anataka kujifungua. Ilibidi sisi kama wawakilishi wadi tuingilie na kumlipia 3600 kutoka kwa mifuko yetu ili aweze kuzalishwa. Kwa hivyo naomba serikali ya kaunti iingilie kati na kuwasaidia watu hawa.

MCA Hope Wanjiku Mwaura (Nominated): Thank you Mr Deputy Speaker Sir, I would like to congratulate Honorable Deko for the noble thought. It is true that the Awere and Sanye communities live in vulnerable conditions. With such conditions, it is very hard for a member of that community to afford quality health care. It is sad that at this age to hear such news. Honorable Deko you have represented your people well and I would urge the House to adopt this motion and the department concerned should work on it very fast to help this community. There is a need for identification and registration for all the Awere and Sanye in Lamu county so that we can get the correct data to help this motion work as soon as possible. If this motion passes, even some of the burden that Honorable Deko goes through will be lifted off his shoulders therefore I am in support of this motion.

MCA Beatrice Wamaitha Munge (Nominated): Thank you Mr Deputy Speaker Sir, my gratitude also goes to Honorable Deko for bringing up this motion to the House. We have marginalized communities like the Awere in Basuba ward not forgetting that they are also in other wards. These people cannot even afford their daily meals as they mostly rely on the wellwishers. They are normally hunters and gatherers and

with the climatic condition which we have, these people deserve good health and protection as per the Constitution of Kenya. The County Government should be able to pay the premium for them as soon as possible. I stand to demand an implementation with an immediate effect.

MCA Shekhuna Abbas Shekhuna (Mkomani): Asante Bwana Spika, nasimama kuunga mkono mswada huu. Kulingana na Katiba 43(1)(a) kila mwananchi ako na haki ya kupata huduma. Kusema kweli jamii hii inapitia changamoto nyingi sana hata wakati wa chakula. Tukumbuke kuwa wale watu walipiga kura wakitegemea kupata huduma kutoka kwa viongozi. Mara nyingi napata changamoto katika wadi yangu hususan katika hospitali ya rufaa ya king na huwa nashirikiana na waziri husika kupambana na mambo kama haya. Kubwa ni kutafakari ni njia gani itatumika kuwasaidia watu hawa. Asante.

MCA Francis Ngure Gakonga (Bahari): Asante Bwana Spika, nasimama kuunga mkono mswada huu. Kwa sababu ya maswala ya bajeti inaweza kuwa ngumu kwa serikali ya gatuji letu la Lamu kuhakikisha kila mtu kupata bima ya afya. Kuna jamii ambazo zinahitaji kupewa kipao mbele kwa sababu hali zao za Maisha ni za chini sana. Bwana Naibu Spika, watu wengi ni maskini na wanashindwa kujilipia huduma za afya katika kaunti yetu. Kuna haja kubwa ya kuhakikisha jamii hizi zinapata bima ya afya ili waweze kufaidika.

MCA Suleiman Mohamed Farah (Witu): Asante Bwana Spika, nasimama kuunga mkono mswada huu. Nasimama kuunga mkono mswada huu. Inasikitisha kwa sababu tangu Kenya ipate uhuru, jamii hii imesahaulika. Katika hali ya usalama ya Lamu, jamii hii iantegemea msitu wa Boni ili kujikimu kimaisha. Vile viel, jamii hii haina uwezo wa kujimudu kulipa bima hio ya SHA. Sisi kama viongozi lazima tuamke kuwasaidia watu hawa kwa hivyo itakuwa vyema ikiwa tutashirikiana na Mheshimiwa Deko kuupitisha mswada huu kwa haraka ili watu wetu wapate kusaidika.

Mover's Response

MCA Barisa Deko Bana (Basuba): Asante Bwana Spika, ningependa kuwashukuru Waheshimiwa wenzangu kwa kuchangia mswada huu. Kusema kweli tangu iletwe mambo ya SHA, jamii yetu ya Awer na Sanye inapata changamoto nyingi sana. Tunashindwa kupeleka watu wetu hospitali kwa sababu tunashindwa kujikimu. Bwana Naibu Spika, tunapata taabu sana na inafaa serikali ya kaunti ishirikiane na serikali kuu ituangalie kwa jicho la huruma. Changamoto ambayo mama wajawazito wanapata imeongezeka kwa asilimia kubwa sana kwa sababu mwaka huu tumepokea akina mama takriban saba ambao wamejifungua kabla ya miezi yao kutimu na wengine hata kupoteza watoto wao. Hali hii mara nyingi husababishwa na mgurumo wa mabomu wa majaribio baina ya wagaidi na maafisa wa usalama wetu. Saa hii serikali imeamua bima ilipwe ya mwaka mzima ambapo hali ya watu kama hawa inazidi kuwa ngumu. Hatuwezi kuingia msitu kama vile tulivyokuwa tukiingia zamani kwa sababu ya hali ya usalama. Kitu kimoja ningependa kushukuru ni kwamba hospitali ya rufaa ya King Fahd inaipa kipau mbele jamii ya Basuba katika huduma bila kuzingatia usajili wa SHA. Binafsi, napokea takribani wagonjwa kumi na tatu kwa wiki ambao wanashindwa kujimudu kiafya. Kama mwakilishi wadi, napata changamoto sana upande wa kupigiwa simu kulipa bili za watu wangu lakini je nitawalipia watu wangapi? Serikali ya kaunti ina uwezo wa kupeana huduma hizi na si Basuba peke ake, waboni wametapakaa kila sehemu Kiunga ikiwa mmojawapo. Viongozi ni lazima watembelee mashinani kujua maisha ya watu kwa sababu kuna wahitaji. Naomba ofisi husika iweze kutekeleza ufichili

wa SHA Kwa jamii ya Boni na Sanye pamoja na wahitaji wengine na iwe imetolewa kwa watu mwafaka wanaostahili. Itakuwa ni vyema iwapo usajili utafanywa basi wajumbe wa eneo hilo wahusishwe ili kuepusha kufanywa kisiasa na pia ningependelea kamati husika bungeni iende mashinani kukagua majina hayo. Vilevile, naomba watu wa huduma za kiafya iwapelekee jamii hizo *mask* ili waweze kujikinga na moshi sumu na maradhi mengine madogo madogo. Naomba wabunge walioko hapa watie manani swala hili na ofisi ya makarani wa bunge waweze kuandika vilivyo na isipungue siku sitini iwe tumepata jibu kamili ili jamii ya Awer na Sanye wawe wamepata huduma ya SHA.

(Question put and Agreed Upon)

ADJOURNMENT

[The Deputy Speaker (Honorable Paul Kimani Njuguna)]: Honorable Members, there being no other business, the Assembly stands adjourned until tomorrow Thursday, Dec 4th, 2025 at 2:30 p.m.

The Assembly rose at 4:15 p.m.